



### Masomo ya Kuogelea wakati wa Likizo

Ni muhimu watoto wako wajifunze kuogelea.

Kunazo fukwe nyingi, mito, mabwawa na shimo za kumwagilia huko Australia Magharibi. Ziko vizuri kwa kucheza, kuogelea na kupoza wakati kuna joto, lakini sio salama ikiwa watoto wako hawawezi kuogelea.

Kujifunza kuogelea humpa mtoto wako ujasiri anapokuwa kwenye maji pamoja na ujuzi wa kuogelea salama.

Watoto wako wanaweza kujifunza kuogelea katika masomo ya kuogelea ya VacSwim ambayo hutolewa wakati wa likizo ya shule ya Oktoba na majira ya joto.

Watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 17 wanaweza kuhusika. Kuna mipango kutoka siku 5 hadi 10. Kuna masomo ya uwezo wote, kutoka kwa wanaoanza kuogelea na wale wazuri.

Masomo ya VacSwim yanapatikana kwa familia nzima na yanapatikana katika mabwawa mengi na fukwe huko Perth na katika maeneo ya mkoa. Tafuta eneo la karibu na wewe kwenye tovuti yetu.

Unahitaji kulipa ada ya uandikishaji ili uandikishe mtoto wako katika mpango. Ikiwa una watoto watatu au zaidi, unaweza kupata punguzo kwa familia yako. Unaweza kuhitaji pia kulipa ada ya kuingia kwenye dimbwi la kuogelea siku hiyo.

Unaweza kupata punguzo ikiwa una moja ya kadi hizi za makubaliano:

- Companion Card
- Commonwealth Seniors Health Card
- Department of Veterans' Affairs Gold, White or Orange
- Health Care Card
- Out of State Seniors Card
- Pensioner Concession Card
- State Concession Card
- WA Seniors Card

Unaweza kuomba kwa:

- tembelea [education.wa.edu.au/vacswim](https://education.wa.edu.au/vacswim) jilandikishe kwenye mtandao, au
- tuma kwa barua pepe au kutoma fomu ya kujiandikisha kwa posta (katika Kiswahili) – inayopakuliwa kwenye tovuti.

### VacSwim 2020-2021

Ratiba ya Oktoba: 29 Septemba – 9 Oktoba 2020  
Oktoba siku 5: 5 – 9 Oktoba 2020

Kuanza Mapema Vijijini: 18 -24 Desemba 2020  
Ratiba ya Januari 1: 29 Desemba 2020 – 8 Januari 2021  
Ratiba ya Januari 2: 11 - 22 Januari 2021

Siku za Januari 5:

4 – 10 Januari 2021

Gharama za VacSwim ni:

Mipango ya Siku 7 hadi 10: Mtoto \$30 (\$20 mwenye punguzo)

Familia \$81 (\$54 mwenye punguzo)

Mpango wa siku 5: Mtoto \$16 (\$10.50 mwenye punguzo)

Familia \$41 (\$27.50 mwenye punguzo)